

YOUTH ACTION VOLUNTEERS

RASIMU YA UPEMBUZI WA BAJETI YA SEKTA YA AFYA 2008/09

1. UTANGULIZI

- Bajeti ya sekta ya afya inachangiwa na fedha kutoka ndani na nje ya nchi. Hapa vipo vyanzo vya ndani (mapato kutokana na kodi, gawio kwa hisa za serikali katika mashirika na makampuni, faini, faida za riba nk) na fedha za nje kupitia katika msaada kwenye bajeti (GBS)
- Hivyo basi bajeti ya sekta ya afya ni majumuisho ya fedha za matumizi ya kawaida pamoja na fungu la fedha za maendeleo.
- Fungu la fedha za matumizi ya kawaida hutokana na fedha kutoka Wizara ya afya na Ustawi wa Jamii, fedha za serikali za mikoaa, fedha za serikali za mitaa na fedha za mfuko wa afya wa wilaya
- Fungu la fedha za maendeleo linajumuisha fedha za ndani na nje kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, fedha za ndani na nje kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, fedha za ndani nje kupitia mikoani na fedha za ndani za serikali za mitaa

2. MUUNDO WA BAJETI YA SEKTA YA AFYA

- Fedha zinazoelekezwa kwenda sekta ya afya hazielekezwi Wizara ya Afya peke yake bali huelekezwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mikoani (kupitia bajeti za afya za Tawala za Mikoa + hospitali za mikoa) na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- Kwa mwaka huu wa fedha 2008/09 fedha zinazokwenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni Jumla ya Shilingi za Kitanzania Bilioni 440 ambapo kati ya hizo Matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 198 na Fungu la maendeleo ni shilingi bilioni 242.
- Tawala za Mikoa imetengewa shilingi bilioni 90 ambapo matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 27; Fungu la fedha za maendeleo kutokana na vyanzo vya ndani ni shilingi bilioni 12 wakati fedha za maendeleo kutokana na vyanzo vya nje ni shilingi bilioni 51.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa (Council health block Grants) katika bajeti ya mwaka huu 2008/09 imetengewa Tsh bilioni 145 na hii ni katika bajeti ja matumizi ya kawaida.
- Angalizo: Vyanzo vya nje katika bajeti ya maendeleo vinajumuisha fedha za nje kupitia msaada kwenye bajeti (GBS) pamoja na mafungu mengine ya fedha za maendeleo. Ingawaje, inaonekana wazi kwamba takwimu hizi zinaweza kuwa na mapungufu. Hii inasababishwa na kujitolea kwa wabia wa maendeleo katika kutoa fedha kwa makubaliano ya awali.

2. MCHANGANUO WA BAJETI YA SEKTA YA AFYA 2008/09


- Sekta ya Afya inaendelea kupewa kipaumbele. Hii ni kutokana na umuhimu wake katika taifa ikihusishwa na uhusiano uliopo kati ya sekta ya afya na sekta nyingine muhimu katika uchumi wa nchi.
- Jumla ya Matumizi katika sekta ya afya kwa mwaka 2008/09 ni Shilingi Bilioni 793,994,300,000 (ambalo ni ongezeko la asilimia 27 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha uliopita)
- Kiasi hiki ni sawa na 11% ya matumizi katika bajeti ya serikali kwa kujumuisha Consolidated Fund Services (CFS) na 12% bila kujumuisha fedha za mfuko wa jumla (Takwimu hizi ni tofauti na Hotuba ya Waziri wa Fedha iliyowakilishwa Bungeni tarehe 12 Juni 2008). Katika hotuba hii, sekta ya afya inaritaarifiwa kutengewa jumla ya shilingi bilioni 803.3 ambapo inaelezwa kuwa ni asilimia 11% ya bajeti nzima ya serikali kwa mwaka wa fedha 2008/09
- Tukirejea mwaka 2007/08 bajeti ya sekta ya afya ilikuwa 10 % na bila kujumuisha CFS ilikuwa ni 11%. Lakini hili linatonesha kinadharia kwamba lipo ongezeko katika sekta hii na hii inlandana ana kwa ana na zana nzima ya kutoa kipaumbele juu ya masuala ya afya. Lakini ukweli ni kwamba bado ni changamoto kwa kuwa haliendani na kushuka kwa thamani ya shilingi na ongezeko la watu kila mwaka.

3. MCHANGANUO WA BAJETI YA SEKTA YA AFYA 2008/09 IKIHUSISHWA NA SEKTA NYINGINE

- Upo uhusiano mkubwa kati ya sekta nzima ya afya na pato halisi la taifa (real GDP). Hii inatusaidia kuwa makini sana pindi tunapopanga mipango yetu ya maendelo. Ni muhimu pia katika kuhakikisha kwamba mikakati mbalimbali tuliyojiwekea kama taifa inafikia malengo.
- Pia upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya sekta ya afya na sekta ya miundo mbinu inayojumuisha mawasiliano na uchukuzi, vile vile sekta nyingine kama vile maji, kilimo, nishati, elimu zina uhusiano wa moja kwa moja na sekta ya afya.
- Uhusiano unaolezwa hapo juu unalenga katika kutetea vipaumbele katika sekta hizo ili kuweza kuboresha sekta ya afya na mapana yake, hivyo basi kufikia lengo la Abuja ambapo ni asilimia 15 ya bajeti nzima bado si hoja inayoweza kuelezea mafanikio katika sekta ya afya. Vipaumbele vinavyowekwa kwa pamoja ndio njia pekee itakayoweza kuboresha sekta ya afya. Kwa mfano: uimarishaji wa njia za mawasiliano kama vile barabara na mawasiliano ya simu yanaweza kuboresha utoaji wa huduma za msingi za afya vijijini ambapo watoa huduma watavutiwa na maeneo ya kazi. Ieleweke wazi kwamba tatizo kubwa linalopewa kipaumbele katika sekta ya afya kwa sasa ni upungufu wa wataalamu katika kutoa huduma za afya.

4. MWELEKEO WA VIPAUMBELE KISEKTA

- Mtiririko wa utoaji vipaumbele kinadharia katika sekta unaonesha kwamba sekta ya afya imekuwa ikipewa kipaumbele kila mwaka. Kwa mfano kuanzia mwaka 2002/03 – 2008/09 sekta ya afya katika bajeti nzima imekuwa ikionyesha mtiririko usiojitosheleza ikilinganishwa na maana halisi ya kupewa kipaumbele.
- Rejea jedwali linaloonesha afya kama sehemu ya bajeti nzima 2002/03 – 2008/09




- Kwa nini mtiririko huo hapo juu hautupi mwelekeo halisi?
Zipo sababu tofauti zinazoweza kuhusishwa na mtiririko huu, na si lazima sababu hizi zikasimama kuwa huru bila kuwa na changamoto. Twaweza kuhusisha sababu za kisera: hizi zinalenga kwenye kuongezeka na kupungua kwa mapato ya ndani na nje; misamaha ya madeni; kukua/kuanguka katika sekta nyingine kwa mfano madini na utalii hivyo kuchangia/kupunguza kwa kiasi kikubwa katika pato la taifa; majanga/matukio mbalimbali; ukame/mvua za kutosha, sera za nchi wahisani wa maendeleo nk
- Changamoto tunayoipitia na inayoonesha wazi kwamba wakati sababu tajwa hapo juu zinaelezea kwa undani juu ya sekta ya afya, kwa upande mwingine sekta ya kilimo inaonesha mtiririko chanya kwa takribani miaka nane sasa. Ukweli ni kwamba sehemu ya kilimo katika bajeti nzima imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka lakini mpaka leo hii, ongezeko hili ni nusu tu ya bajeti afya kwa mwaka na changamoto kubwa ni pale tunaposhindwa kuhusisha vipaumbele vya kissekta vinavyoshabihiana kwa njia moja ama nyingine. Kwa mfano sekta ya kilimo inachukua asilimia 70 ya watanzania wote, ikiwa na maana ya kuwepo uhusiano wa sekta ya afya na kilimo. Huu ni uhusiano mkubwa na zaidi ya hapo katika mwaka 2008 takwimu zinaonesha kwamba sekta ya kilimo ikijumuishwa na

uwindaji pamoja na misitu inachangia asilimia 26 ya pato halisi la taifa. Hii ndio sekta pekee yenye asilimia kubwa katika pato la taifa. Nguvu kazi bila afya bora haileti tija. Utetezi wa bajeti zinazoendana moja kwa moja na matumizi yanayozingatia kanuni na taratibu sahihi za kiutendaji ni muhimu.

- Rejea jedwali lifuatalo

Jedwali 1: Bajeti ya Sekta ya Kilimo (2000/01 – 2008/09)



Source: Various Economic Surveys and Reports (URT)

5. MATOKEO YA UPEMBUZI

- Jumla ya bajeti ya afya imeongezeka. Haya ni mafanikio makubwa sana. Hii inaonesha jitahada za kuipa sekta hii kipaumbele.
- Ongezeko katika mikoa linaonekana katika bajeti ya mwaka huu. Tunatarajia uboreshwaji wa huduma katika ngazi hii pamoja na ufanisi wenye tija. Ongezeko hili ni kubwa sana. Asilimia 751 ya rasilimali fedha kuelekea mikoani inatupa mashaka katika suala zima la matumizi yake. Uwajibikaji na utawala bora katika sekta hii bado ni changamoto kubwa. Maelezo zaidi yanapatikana katika `Matokeo ya Upembuzi – Medium Picture`.
- Pia lipo ongezeko chanya katika mamlaka za serikali za mitaa

Jedwali 2: Mabadiliko katika Matumizi (2006/07 – 2008/09)

	Mabadiliko katika Matumizi			
	2008/09	2007/8	% Badiliko	2006/7

Wizara ya Afya	439,685.0	369,564.0	19	286,840
Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	25,027.0	2,942.0	751	22,436
Mikoa	89,386.0	72,718.0	23	23,849
Serikali za Mitaa	239,896.3	182,061.0	32	158,716
Jumla	793,994.3	627,285.0	27	491,841

Matokeo ya Upembuzi – Medium Picture

BAJETI YA SEKTA YA AFYA 2008/09 - MEDIUM PICTURE

Recurrent	Bajeti ya 2005/06	Bajeti ya 2006/07	Bajeti ya 2007/08	2008/2009	Ongezo/ Upungufu	% Badiliko
Mhasibu Mkuu (Bima ya Afya ya Taifa)	20,457	29,550		0		0.00
Wizara ya Afya (Serikali .)	180,306	195,981	187,628	198,118	10,490	5.59
<i>of which Personal Emulment</i>	6,407	17,473	16,005	18,827	2,822	17.63
<i>of which OC</i>	173,899	178,509	171,623	179,291	7,668	4.47
Tawala za Mikoa	11,532	18,978	28,761	27,164	-1,597	-5.55
Mamlaka za Serikali za Mitaa	95,389	135,622	137,700	144,792	7,092	5.15
Pesa za Serikali	75,314	112,528				0
Fedha za Mfuko wa Wafadhili	20,075	23,094				0
Total Recurrent	307,684	380,131	354,089	370,074	15,985	4.51
<i>Total Recurrent excl NHIF</i>	<i>287,227</i>	<i>350,581</i>	<i>354,089</i>		<i>3,508</i>	<i>1.00</i>

Maendeleo	2005/06 Budget	2006/07 Budget	2007/08 Budget	2008/09 Budget	Increase / Decrease	% Change
Wizara ya Afya	90,863	90,859	181,936	241,567	59,631	33

Fedha za Serikali	5,000	7,123	6,774	13,029	6,255	92
Fedha za Mfuko wa Serikali	28,486	20,400	104,303	124,602	20,299	19
Fedha za Nje (Sio za Mfuko)	57,377	63,336	70,859	103,936	33,077	47
<i>Foreign Jumla Total</i>	85,863	83,736	175,162	228,538	53,376	30
Ofisi ya Waziri Mkuu , Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa	19,838	22,436	2,942	25,027	22,085	751
Fedha za Serikali	100	70	0	23,000	23,000	0
Fedha za Mfuko wa Wafadhili	19,738	12,990	450	650	200	44
Fedha (Sio za Mfukot)	-	9,376	2,492	1,377	-1,115	-45
Mikoa	5,049	4,871	43,957	62,222	18,265	42
Fedha za Serikali	1,169	2,277	7,330	11,703	4,373	60
Nje (Sio za Mfuko)	3,880	2,594	36,627	50,518	13,891	38
Mamlaka za Serikali za Mitaa	20,137	23,094	44,361	95,104	50,743	114
Fedha za Serikali	2,579	2,500			0	0
Fedha za Nje					0	0
Jumal ya Fedha za Maendeleo	118,329	120,666	273,196	423,920	150,724	55
Mamlaka za Serikali za Mitaa 95,104 Hazionekani katika vitabu vya bajeti						

- Matumizi ya kawaida yanaonekana kuongezeka kwa asilimia 4.5 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2007/08. Fedha za mishahara zimeongezeka kwa asilimia 17 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hii inaweza ikawa inatuashiria ongezeko la rasilimali watu katika sekta ya afya na vile vile inaweza kuwa ni ongezeko katika mishahara katika kuboresha sekta ya afya. Haya yote hayawezi kuwa majibu toshelezi, tunahitaji kuona MTEF ya wizara ya afya inasemaje juu ya sekta hii. Hii itatusaidia kuondoa mashaka ya uwezekano wa kuwepo ajira hewa katika sekta hii. Matumizi ya kawaida yameongezeka kwa asilimia 4.5. Changamoto kubwa inakuja katika matumizi sahihi ya rasilimali hizi. Ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinatupa picha yenye mashaka juu ya matumizi sahihi ya rasilimali fedha katika sekta hii.
- Matumizi fungu la fedha za Maendeleo yanaonekana kuongezeka kwa asilimia 55 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita. Tunapata mashaka sana kuona ongezeko kubwa kiasi hiki wakati tukiwa na vielelezo vinaovyoonesha ufanisi duni kwa mwaka 2007/08. Tukireje Health Sector PER Update 2007 ya Wizara ya Afya katika ukurasa wa 11 tunaona kwamba fedha zilizopelekwa mikoani kwa mwaka huo kwa ajili ya matibabu zilitumiwa kwa kiasi cha asilimia 27 ambacho ni sawa na shilingi bilioni 4.2 tofauti na shilingi bilioni 15.4 kiasi kichopitishwa katika bajeti. Hii inatuonesha kwamba katika mikoa kiasi kikubwa cha fedha hakiwezi kutumiwa kwa malengo yaliyoainishwa, labda rasilimali watu haitoshelezi na zaidi yawezekana kabisa ujuzi ni mdogo sana. Swali la kujiuliza ni kama ongezeko hili katika mikoa litaweza kuleta tija katika kuboresha sekta ya afya. Na je dhana nzima ya utawala bora itatekelezeka?
- Kwa kufuata misingi ya kisera, tunajua wazi ongezeko hili linaenda sambamba na jitihada za serikali kupeleka madaraka mikoani. Hivyo basi tunahitaji kuwa na njia au mbinu mbadala katika udhibiti wa rasilimali katika tawala za mikoa na wilaya.
- Changamoto: Rasilimali watu katika sekta ya afya ni tatizo kubwa sana. Ila inashangaza kuona katika ripoti ya Health Sector PER 2006/07 ukurasa wa 11, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya maendeleo ya rasilimali watu katika Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii kilitumia asilimia 23 tu ya fedha zilizopitishwa katika mwaka wa fedha 2006/07. Hii inahusisha udhaifu na mapungufu katika kutekeleza mipango iliyopangwa labda kwa kutokuwa na wataalamu wa kutosha ama sababu nyingine yoyote.
- Upembuzi wa MTEF unaonesha kwa mwaka 2006/07 ni asilimia 49 ya mipango iliyokuwa imepangwa mwaka ule katika fungu la fedha za maendeleo ndiyo iliyotekelezeka. Inawezekana kuwa bajeti hii ya maendeleo ikawa inakosa mafungu ya fedha yaliyoahidiwa na wahisani na hivyo kurudisha nyuma mipango yetu ya maendeleo, hivyo basi hatuna budi kuwa na njia thabiti zitakazoweza kuwabana wahisani na wabia wetu wa maendeleo juu ya ahadi wanazozitoa kwa

ajili ya kusaidia bajeti zetu. Angalizo la vipaumbele ni vyema likaangalia rasilimali halisi zilizopo na kuachana na dhana kutumia bajeti picha (theoretical commitment)

- Kiasi cha fedha kinachoenda hospitali za mikoa kinaonesha kwamba baadhi ya mikoa haijatengewa fedha. Kwa mfano mkoa wa Tanga, Tabora na Dar es Salaam.

6. CHANGAMOTO KUTOKANA NA UPEMBUZI WA BAJETI YA MWAKA 2008/09

- Usahihi wa takwimu za bajeti bado ni tatizo. Tunapata mashaka na wataalamu wanaondaa bajeti kwamba inawezekana wanatumia takwimu za miaka iliyopita bila kurejea mipango kazi na mpango mkakati unaoongoza sekta ya afya pamoja na vipaumbele vyake. Kiasi kilichotengwa kwa ajili ya bima ya Afya, kitabu namba 3 cha bajeti, kupitia voti ya mhasibu mkuu inaonekana kama `contribution to pensions and welfare for 2007/08 as Tsh 30,177 billions) na kiasi hiki katika kitabu na IV hakimaanishi Bima ya Afya ya Taifa, bali takwimu hizi katika MTEF ya mwaka huo ndizo zinaonekana kama fedha kwa ajili ya MTEF. Kama hilo si tatizo basi tunajiuliza kwa nini kiasi hicho hicho kinaonekana katika bajeti ya mwaka 2008/09? Je, hamna badiliko katika rasilimali watu? Hamna punguzo wala ongezeko?
- Imekuwa ni kilio cha miaka mingi sasa, tunasema huduma ya mama mjazito na mtoto chini ya miaka 5 inatolewa bure. Hivi ndivyo maelekezo ya serikali yanavyosema lakini swali linakuja ni wapi katika bajeti ya afya haya yameainishwa? Na pia hata kwenye sera ya Afya ya Kitaifa halijaainishwa. Bado tunasikia malamiko kila kukicha akina mama wanakosa huduma katika vituo vya afya, akina mama wanatakiwa kwenda na vifaa vya kujifungulia' katika vituo vya afya. Je, maelekezo ya serikali yanaendana na vipaumbele vilivyowekwa katika sekta ya afya? Ni wapi katika bajeti tunaweza kuona watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wazee na walemavu wamekuwa na fungu lao katika afya?
- Bajeti ya mwaka wa fedha 2007/08 ilitenga kiasi cha shilingi za Kitanzania billioni 1.7 kununua pikipiki 222 za magurudumu matatu kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa wagonjwa katika maeneo yenye miundombinu mibovu ya barabara. Taarifa zilizopo zinaonesha kwamba pikipiki hizi hazikununuliwa na hakuna maelezo ya kuridhisha. Pia kwenye bajeti ya mwaka 2008/09 hazijatengewa pesa. Hivyo basi;

- Umuhimu wa ufuatiliaji na utekelezaji wa mipango ya mwaka wa fedha uliopita. Hii itasaidia kupitisha bajeti zenye tija na zinafuatilia vipaumbele

Uzoefu katika Wizara ya Afya kuanzia 1999 (billions)


A	B	C	D	E
Mwaka	Bajeti	Mkaguzi Mkuu	Kiasi kisichotumika	Tofauti B ajeti – Mkaguzi Mkuu
1999/2000	88.7	24.3	18	70.7
2000/01	118.76	26.3	16	102.76
2001/02	151.04	7.0	17	134.04
2003/03	192.77	7.2	18	174.77
2003/04	201.02	17.1	0	201.02
2004/05	308.28	31	20	288.28
2005/06	425.77	8.93	42	383.77

2006/07	521.07	9.76	94	427.07
Jumla	2,007.41	131.59	225	1782.41

Chanzo: Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii MoHSW PER Updates

- Ripoti za Mkaguzi Mkuu zina taarifa muhimu sana katika utekelezaji wa mipango ndani ya sekta ya afya na sekta nyingine. Ni vyema sana mapendekezo ya ripoti hizi kupewa kipaumbele kabla ya kupitisha bajeti ya sekta yoyote ile.
- Ushirikishwaji wa watunga sera katika ufuatiliaji na tathmini ya mipango kazi ya sekta (Kuzipitia sheria zetu na kuweza kutengeneza nafasi kwa ajili ya watunga sera kushiriki katika mchakato mzima wa Upangaji rasilimali, usimamiaji wa matumizi, usimamiaji wa utendaji, Performance Management, Public Integrity and Oversight bodies)
- Rasilimali katika sekta binafsi zinakwenda wapi? Mchango wa sekta binafsi utambuliwe kwa mapana yake. Maswala ya utawala bora katika sekta hii hayana budi kufuatiliwa kwa umakini zaidi ili kuweza kutathmini mchango wa sekta hizi katika utekelezaji wa sera za taifa.
- Vipaumbele katika bajeti ni jambo muhimu sana. Ni kweli yapo mambo ambayo yangeweza kupewa nafasi kwa kipindi kijacho na mengine ambayo ingekuwa ni busara sana kuyatekeleza kwa sasa kwa mfano ujenzi wa nyumba moja ya spika (Bilioni 2.3 katika Vote 42) gharama ambayo inaweza kujenga takribani zahanati 10 zenye idara ya wagonjwa wa nje, idara ya huduma ya afya ya mama na mtoto, idara ya kina mama wajawazito, vyoo vya nje, tanuru la kuchomea taka hospitali, nyumba 2 za wafanyakazi kwa ajili ya familia 3.
- Uwiano kati ya uhitaji na vipaumbele ni muhimu sana. Tofauti za upelekwaji rasilimali fedha na rasilimali watu kati ya sehemu moja na nyingine ni muhimu sana. Kwa nini mkoa mmoja upewe kipaumbele tofauti na mkoa mwingine bila kuangalia uhitaji?

Amount Going to Regional Hospitals in each Region 2008/2009



- Umuhimu wa kuhakikisha vipaumbele kisékta unakwenda kwa pamoja ni muhimu katika kuboresha sekta ya afya. Kwa Mfano Wizara ya elimu inajukumu la kutoa mikopo kupitia bodi ya mikopo hivyo basi ni vyema tuangalie wahudumu wetu wa afya wanaosomeshwa katika sekta ya elimu wanakidhi uhitaji na nini kifanyike tukizingatia elimu na afya kwa pamoja ni sekta muhimu zinazopewa vipaumbele?
- Ni kwa nini suala zima la vifaa na madawa limekuwa kero? Tunaona kiasi kikubwa cha fedha kinatengwa kwa ajili ya MSD lakini bado kuna upungufu mkubwa na hivyo kuwa kero kwa wananchi?
- Kwa nini watoa huduma wa sekta binafsi wana maadili mazuri tofauti na watoa huduma katika sekta ya umma? Je ni kukosekana kwa maadili ndani ya sekta ya umma? Kama ndivyo maadili ya watumishi wa umma na hapa tukirejea watoa huduma za afya wanawajibishwa vipi na taratibu zilizopo? Nachele kusema maadili ni mazuri katika sekta binafsi bali tunganisite uwajibikaji na mfumo wa kutoa malalamiko na taratibu zingine zilizopo kama zinakidhi mahitaji ya watoa huduma za afya. Wengi walio katika sekta binafsi wanatumikia hata kwenye serikali

REJEA

1. Health Sector PER Update 2007, Ministry of Health and Social Welfare
2. Controller and Auditor General reports from 1999 to 2008
3. Various Economic Surveys and Reports (URT)
4. Vitabu vya Bajeti 2007/08
5. Vitabu vya Bajeti 2008/09